KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

25/= Ksh

Volume 24, Issue 3

8th Ramadhaan 1433

27th JULY, 2012

RAMADHAAN - UKUMBUSHO WA UMOJA

NA: SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI (رحمه الله)

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA LEO

RAMADHAAN—UKUMBUSHO… 1 - 2

QIYAAM UL-LAYL 2 - 3

Amepokea Abu Hurairah yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): **"Funga pindi watakapoanza kufunga, na ufungue saumu watakapomaliza saumu zao, na uchinje katika siku watakapochinja."**

Amepokea al-Bayhaqee kwa kupitia kwa Abu Haneefah, aliyesema: 'Alee ibn al-Aqmar amenisimulia, kutoka kwa Masrooq, aliyesema: Niliingia kwenye nyumba ya 'Aaishah katika siku ya 'Arafah, akaniambia: "Muandalie Masrooq ubwabwa (uji), ufanye uwe na ladha nzuri." Akasema Masrooq: Hakuna kilichonizuiya nisifunge leo isipokuwa nilikuwa nikihofia isije ikawa ni siku ya kuchinja (Siku ya 'Idd ul-Adh-ha). Basi 'Aa'ishah akaniambia: "Siku ya kuchinja ni siku watu wanapochinja, na siku ya kumaliza kufunga ni siku watu watakapomaliza kufunga." Silsila hii ya riwaya ni jayyid (nzuri) kutokana na yaliyotangulia.

KATIKA UFAHAMU WA HADEETH HII:

Imaam at-Tirmidhee amesema baada ya kuinukuu hadeeth hiyo: Mmojawapo wa wanavyuoni ameifafanua hadeeth hii kwa kusema: Maana yake ni kufunga na kumaliza kufunga pamoja na Jamaa'ah na kundi kubwa la watu."

As-San'aanee akasema katika Sublus-Salaam (2/72): "Katika hadeeth hii kuna dalili yakwamba kuafikiyana na watu ni jambo linalokubalika katika kuithibitisha 'Eid, na kwamba mtu mmoja peke yake anayeamini yakwamba ni siku ya 'Eid - kwa sababu kuuona mwezi - basi ni waajib juu yake akubaliane na watu na kwamba kukatikiwa kwa watu, kuhusiana na swala, kufungua saumu na kuchinja yatampasa mtu binafsi."

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) ameitaja maana hii katika Tahdheebus-Sunan (3/214), kisha akasema: "Imesemwa: Ndani yake wamesutwa wale wenye kusema, 'yoyote mwenye kujua mahali ulipo mwezi kutokana na hesabu za uta'alamu wa ilmu ya nyota, basi ataruhusiwa kufunga na kufungua, hata kama wengine hawatojua. Vilevile imesemwa: Yakwamba shahidi mmoja mwenye kuuona mwezi, lakini Kadhi akamkanusha kuhusu ushahidi wake huo, basi hapatokuwa na saumu kwake kama kwamba hapatokuwa na saumu kwa watu."

Amesema Abul-Hasan as-Sindee katika Haashiyah 'alaa Ibn Maajah, baada ya kuitaja hadeeth ya Abu Hurayrah iliyopokewa na at-Tirmidhee: "Na maana yake yenye kudhihiri ni: Kwamba hakuna nafasi kwa (rai ya) mtu yoyote kuyaingilia mas'ala haya, wala mtu kujifanyia atakavyo. Bali haya mas'ala hurudishwa kwa Imaam (kiongozi wa Waislamu) na jamaa'ah (kundi lililoundwa la Waislamu wakiwa chini ya Imaam). Ni waajib kwa mtu binafsi kuwafuata kundi hilo na Imaam. Kutokana na haya ni kwamba iwapo mtu atauona mwezi, lakini kadhi akaukataa ushahidi wake, basi mtu huyo hatokuwa na haki katika mas'ala haya, na badala yake itambidi afuate jamaa'ah katika uamuzi huo."

Na hii ndiyo maana iliyodhihiri kutoka katika hadeeth hiyo na ndiyo iliyotiliwa mkazo na ukweli yakwamba 'Aa'ishah (رضي الله عنها) aliitumia pamoja na Masrooq alipojizuiya kufunga katika siku ya 'Arafah, akihofia isije ikawa ni siku ya kuchinja (Adh-ha). Kwahivyo akamueleza yakuwa hakuna uzito wowote uliopewa katika rai yake katika suala hilo, na kwamba na afuate jamaa'ah. Kwahivyo akamwambia: "Siku ya kuchinja ni siku watu wanapochinja, na siku ya kumaliza kufunga ni siku watu watakapomaliza kufunga."

(Endelea kwenye Uk. 2)

HABARI ZA MJI KWA MUKHTASAR

IDADI YA WALIOFARIKI ZANZIBAR YAZIDI 30

Takriban watu 30 wamefariki dunia baada ya meli iliyokuwa imewabeba abiria zaidi ya mia mbili na hamsini kuzama karibu karibu na kisiwa cha Zanzibar nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa zilizitolewa na kikosi cha wanamaji, watu wengine wengi wanaripotiwa kuokolewa kufuatia meli hiyo kuzama kutokana na dhoruba kali.

Mmoja wa watu waliofika katika eneo kulikotokea ajali hiyo na kushiriki katiia uokoaji ni Mohammed Omar ambaye aliambia BBC kuwa meli hiyo ilikuwa imepinduka na injini zake zikiwa juu: "wengi wa waliookoka ni wale wanaojua kuogolea vivi hivi na Mwenyezi Mungu."

Mwandishi wetu wa Dar Es Salaam, Hassan Mhelela, ambaye amekuwa akifuatilia ajali hiyo tangu itokee jana

(Endelea Uk. 4)

(Endelea Kutoka Uk. 1)

UMOJA NI MOJAWAPO YA MALENGO YA SHAREE'AH:

Na hili ndilo linalostahili kwa Sheriya yenye usahali na usamehevu mzuri, mojawapo ya malengo ambayo ni kuwaunganisha watu pamoja, kuweka sawa swafu zao na kuziepusha mbali na kila lenye kuwatenganisha katika umoja wa maarifa - kutokamana na rai za ubinafsi. Kwahivyo Sheriya haiweki uzito wowote kwenye rai za ubinafsi zinazohusu mas'ala ya Ibaada Jamaa'iyyah (Ibada za umoja), kama vile kufunga, kuswali 'Eid kwenye swala ya Jamaa'ah, hata kama rai ya mtu iko sawa, kwa upande mmoja. Kwani wewe huoni vipi Maswahaba (رضي الله عنهم) walivyokuwa wakiswali mmoja nyuma ya mwengine. Sasa kutokamana nao ni wale wenye maoni yakwamba kumgusa mwanamke, au kutokwa na damu mwilini hutangua wudhoo', pamoja na wale wenye msimamo mwengine. Miongoni mwao ni wale wenye kukamilisha swala zao wanapokuwa kwenye safari, haliyakuwa wengine hufupisha swala zao. Sasa tafauti hizi na nyenginezo, hayakuwazuiya kuswali kwa pamoja nyuma ya Imaam mmoja kuashiriya yakwamba ni mambo yanayoruhusiwa. Na hii ni kwa sababu walikuwa wakijua yakwamba tafarruq (kutengana) katika mas'ala ya dini ni uovu zaidi hata kuliko kuwa na ikhtilaaf (tafauti) kwenye baadhi ya rai. Kwa hakika mas'ala na mmoja wao yalifikia kiasi cha kwamba hata hakuweza kukubali au kuiruhusu rai yoyote inayokwenda kinyume na ma-Imaam wakubwa kwenye mikusanyiko mikubwa; kama vile mkusanyiko wa mahujaji kwenye uwanja wa minaa; kwa kiasi cha kwamba atatupilia mbali utekelezaji wa rai zake alizokuwa nazo kwenye mikusanyiko hayo - akijiweka kando na hilo lenye kuweza kuleta maafa kutokana na uovu huo, kwa sababu ya kutekeleza mambo kulingana na maoni yake. Kwahiyo, amepokea Abu Daawud (1/307) yakwamba 'Uthmaan (رضي الله عنه) aliswali raka'a Nne alipokuwa yuko Minaa, basi Abdullaah Ibn Mas'ud akamlaumu na akamwambia: "Mimi niliswali raka'a mbili na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na raka'a mbili na Abu Bakr (رضي الله عنه), na raka'a mbili na 'Umar (رضي الله عنه) na raka'a mbili na 'Uthmaan (رضي الله عنه) alipokuwa kwenye mwanzoni mwa utawala wake, kisha akaikamilisha (yaani kwa kuswali raka'a nne). Baada ya hapo nyinyi mukaanza kuzigawanya njia. Kwahiyo, natumai kutokana na raka'a nne hizi, yakwamba raka'a mbili zitakubalika." Kisha Ibn Mas'ud akaswali raka'a nne. Basi akaambiwa: "Wewe umemlaumu 'Uthmaan, kisha ukaswali raka'a nne, ni kwanini?" Nae akajibu: "Kukhitilafiana ni uovu."

Silsila yake ya upokezi ni swaheeh, na jambo jengine linalofanana nalo limepokewa kwenye Musnad (5/155) cha Imaam Ahmad, kutoka kwa Abu Dharr (رضي الله عنه).

Kwahivyo wale wenye kuendelea kuwagawanya watu kuhusiana na mas'ala ya swala, na wenye kukataa kuwafuata ma-Imaam wa mijini mwetu katika baadhi ya misikiti - hususan katika swala ya witr, mwezi wa Ramadhaan, wakitumia kuwa ni dalili ati haya ni kinyume cha madh-hab yao, basi na waizingatie hadeeth hiyo iliyotangulia na aathaar. Vilevile, wale wenye kujidai kuwa wana ilimu ya mas'ala ya nyota na ambao, kutokana na rai zao, wanafunga, hufunga na kumaliza saumu zao peke yao wakiwatangulia au wakibakishwa nyuma na kundi kubwa la Waislamu, wasione matatizo yoyote kwa kufanya hivyo - wanatakiwa vilevile wazingatie dalili zilizotajwa hapo awali. Kwahivyo, wote hao na waizingatie na kuitafakari ilmu iliyotajwa. Labda watakuja kujionea wenyewe tiba ya ujinga wao na kujidanganya, kwahivyo, hapo huwenda wakawa ni swafu moja iliyoungana pamoja na ndugu zao Waislamu - kwani kwa hakika Mkono wa Allaah (سبحانه وتعالى) uko juu ya Jamaa'ah.

VIDOKEZI 7 VYA KIUTENDAJI KWA AJILI YA KUSWALI *Qiyaam Ul-Layl*

Muhammad Nasir ud-Deen al-Albanee (*rahimahullah*)

NI NINI QIYAAM UL-LAYL:

Maana ya Qiyaam' ni 'kusimama' na 'Qiyaam ul-Layl' maana yake ni 'kisimamo cha usiku.' Katika matumizi ya lafdhi za kisheriya, matamshi yote mawili yanahusiana na, 'swala ya Sunnah ya usiku, ambayo wakati wake huanzia baada ya swala ya 'Ishaa' mpaka mapambazuko ya alfajiri.' Majina mengine maarufu ya Qiyaam ul-Layl ni, Swalaat ul-Layl (swala ya usiku), Tahajjud (limetokana na hajada lenye maana ya kukesha usiku), Witr (idadi isiyogawika kwa mbili, pia inatumika kuihusu raka'a ya mwisho au tatu za mwisho za Qiyaam) na Taraweeh (mapumziko).

Kutoeleweka kukubwa ni kwamba Tahajjud ni swala tafauti ya usiku isiyokuwa Qiyaam au Taraweeh. Ni muhimu kupambanua ukosefu huu wa ufahamu na kuweka wazi yakwamba kuna swala moja tu ya nafl ya usiku inayojulikana kwa majina tafauti. Hata kama neno "taraweeh" ndilo linalojulikana kwa kawaida katika kuieleza swala ya usiku katika mwezi wa Ramadhaan, haina tafauti na Tahajjud. Kwahiyo, mazoweya ya kuswali Taraweeh katika nyakati za mwanzo wa usiku na tahajjud katika nyakati za mwisho wa usiku yanafaa kukomeshwa.

FADHLA ZA QIYAAM UL-LAYL:

Ahaadeeth nyingi na aya za Qur'aan zimetaja fadhla za Qiyaam ul-Layl na malipo ya wenye kudumu kuitekeleza. Ummul Mu'mineen, 'Aaisha (رضي الله عنها) amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "'Amali zinazopendekeza zaidi mbele ya Allaah ni zile zenye kudumu, hata kama ni chache." [Swaheeh al-Bukhaari na Swaheeh Muslim] na akasema tena katika riwaya nyengine: "Usiwache kabisa kuswali Qiyaam. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwacha kuswali swala hiyo. Pindi alipokuwa ni mgonjwa au alipodhoofika, aliiswali kwa kukaa." [Swaheeh al-Bukhaari na Swaheeh Muslim]. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Fanyeni muswali Qiyaam ul-Layl kwani ni tabia ya watu wema waliokuja kabla yenu, na itawasongeza karibu ya Mola wenu, na kuwafutia madhambi yenu, na itawakinga na madhambi, na kuwaondolea maradhi kutoka kwenye miili yenu." [At-Tirmidhee and Musnad Ahmad].

Mu'aadh Ibn Jabal (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia: "Basi nisikuonyeshe milango ya kheri?' (nayo ni), " (a) Kufunga ni kinga ya moto, (b) As-swadaqah huzima madhambi, kama jinsi maji yanavyozima moto, (c) kisimamo cha kwenye swala kinachotekelezwa na mja wa Allaah katika wakati wa thuluthi tatu za mwisho wa usiku. Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaisoma aya isemayo: "**Huinuka mbavu zao kutoka vitandani wakati**

wa usiku ili kumuabudu Mola wao kwa kuogopa Moto na kutaraji Pepo, na hutoa (Zaka na Swadaka) katika yale tuliyowapa." [as-Sajdah 32:16; Abu Daawud na at-Tirmidhee]

Abu Hurairah (رضي الله عنه) amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Swala iliyo bora zaidi baada ya zilizofaradhishwa (za waajib) ni zile za kwenye masaa ya usiku mkubwa." [swaheeh Muslim].

Abu Hurairah (رضي الله عنه) amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Allaah na amrehemu mume mwenye kuamka usiku, akaswali, na akamuamsha mkewe aswali; na lau atakataa (huyo mke) kuamka, humnyunyizia maji kwenye uso wake. Na Allaah amrehemu mwanamke mwenye kuamka usiku, akaswali, na akamuamsha mumewe aswali; na lau atakataa (huyo mume) kuamka, humnyunyizia maji kwenye uso wake." [(Hasan) Abu Dawood]

Amepokea Abdullaah Ibn Bashr (رضي الله عنه) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yoyote mwenye kuswali Qiyaam na akasoma aya kumi, basi hatoorodheshwa pamoja na wenye kughafilika. Yoyote mwenye kuswali Qiyaam na akasoma aya mia moja, ataorodheshwa pamoja na wenye juhudi . Na yoyote mwenye kuswali Qiyaam akasoma aya elfu moja, basi ataorodheshwa pamoja na wale wenye amali nyingi nzuri." [(Hasan) Abu Dawood]

MAWAIDHA KWA NJIA YA DVD

YA QSSEA PRODUCTION

Sasa unaweza kujipatia DVD na kusikiliza Mawaidha kutoka **QSSEA**

- Ruqya ya kisheriya
- Jinsi ya kuosha Maiti
- Hukmu za Sihr
- Mambo Yenye kubatilisha Imani ya Mtu
- Malezi Bora katika Uislamu

Na nyenginezo.

Piga simu Nambari 0721473181

1: IKHLAS - UFUNGUO WA KUNAKO MSAADA WA ALLAAH NA BARAKA ZAKE

Msaada wa Allaah unahitajika katika kukamilisha na kujipatia kufuzu kwenye hali zetu. Na Allaah huwasaidia wenye ikhlaas katika nyoyo zao. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Lau kama wewe ni mkweli mbele ya Allaah, basi Allaah atakuteremshia utakalo au utamanilo. [An-Nasa'ee, al-Hakim na Swaheeh al-Jamee]. Kwahivyo, inatakiwa mtu awe na niya kwa ikhlaas ya kuswali Qiyaam ul-Layl; atafute radhi za Allaah Peke Yake na ajiepushe na matamanio ya kusifiwa au umaarufu. Amesema Allaah: **"Wala hawakuamrishwa ila kumuabudu Allaah Peke Yake..."** [al-Bayyinah (98): 5].

Amesema Imam Ibn al-Qayyim: "Daraja inayompasa mtu kupata msaada na kuokolewa na Allaah hutegemea kiwango chake cha niya yake, malengo, na matarajio. Msaada wa kutoka kwa Allaah huwajilia watu kwa viwango vya kupishana kwenye malengo, matarajio na niya zao, na kutofaulu kwao huwajia kwa njia kama hiyo."

2: KUZIJUA FADHLA ZA QIYAAM UL-LAYL

Kuzijua fadhla na malipo ya kutekeleza ibaada huzalisha kuridhika na mapenzi ya kufanya ibaada. Tumetangulia kuzitaja fadhla chungu nzima za kudumu kuswali Qiyaam ul-Layl, hapa tumetaja ubora wa kuswali Qiyaam ul-Layl hususan katika mwezi Mtukufu wa Ramadhaan

Abu Hurairah (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم)

FUNGUA SAUMU

USIFUNGUE MUADHINI!

SISI HATUFUNGUI MUADHINI KWA SABABU MUADHINI HAUFUNGWI BALI TWAFUNGUA SAUMU KWA SABABU TWAFUNGA SAUMU.

amewahimiza watu pasi na kuifanya kuwa ni amri ya lazima, kuswali Qiyaam katika mwezi wa Ramadhaan. Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: "Yoyote mwenye kusimama (kwenye Qiyaam) katika mwezi wa Ramadhaan kwa Imani na matumaini (ya malipo ya kutoka kwa Allaah), basi atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia." [Swaheeh Muslim].

3: USINGIZI KIDOGO WAKATI WA MCHANA

Kujipatia usingizi kidogo kabla au baada ya swala ya adhuhuri huondoa kero la moyo, na kwahiyo humuwezesha mtu kuamka katika wakati wa usiku akasimama mbele ya Mola wake. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Jipumzisheni na usingizi, kwani Sheitwaan hajipumzishi na usingizi." [Imepokewa na at-Tabaranee. Al-Saheehah (2647)]

4: KULALA KULINGANA NA SUNNAH ZA MTUME WA ALLAAH

(a)Kulala mapema ni mazoweya ya kujenga afya bora na ndiyo tabia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kulala moja kwa moja pindi tu umalizapo swala ya 'Ishaa' Abu Barzah al-Aslami (رضي الله عنه) alisema yakwamba Mtume alikuwa akipendelea kuichelewesha swala ya 'Ishaa', na hakupenda kulala kabla ya kuiswali swala hiyo. [Swaheeh al-Bukhaari].

(b) **KULALA UKIWA KATIKA HALI YA TWAHARA:**

Ibn Abbas (رضي الله عنه) amepokewa akisema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Itakaseni miili hii na Allaah Atawatakaseni nanyi, kwani hakuna mja atakaekwenda kulala akiwa kwenye hali ya utakaso, isipokuwa Malaika ataupitisha wakati pamoja nae, na kila atakapogeuka, [Malaika] atakuwa akisema, "Yaa Allaah! Msamehe mja wako, kwani amekwenda kulala akiwa kwenye hali ya twahara.'" [Imepokewa na at-Twabaraani. Pia angalia kwenye Swaheeh al-Jaami' (3831)]

(c) TAFUTA KITANDA KIZURI:

Starehe za kupindukia mipaka au vitanda vilivyo nyororo husababisha uvivu na humfanya mtu azidishe usingizi wake na akawa ni mwenye kupuuza ibaada. 'Aaisha (رضي الله عنها) amesimulia yakwamba mto aliokuwa akiulalia Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakati wa usiku ulikuwa umetengezwa kwa ngozi na mti wa jamii ya mchikichi." [Abu Daawud na Musnad Ahmad. Swaheeh al-Jamee (4714)]

Siku moja, 'Umar Ibn al-Khattab (رضي الله عنه) aliingia nyumbani kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), akamkuta amelala (amejinyosha) kwenye mkeka uliotengenezwa kwa mti wa jamii ya mchikichi. Akawa amefanya alama kwenye ngozi yake. 'Umar akamwambia "Ewe Mjumbe wa Allaah! Kwanini huangalii kitu chengine kizuri kuliko hiki?" Akamjibu Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mimi nna nini na ulimwengu huu? Uhusiano wangu na ulimwengu huu ni kama wa msafiri katika siku ya kiangazi,

(Endelea kwenye Uk. 4)

(Endelea kutoka Uk.. 3)

mwenye kujitafutia kivuli chini ya mti kwa kiasi cha saa moja, kisha akaondoka na kuendelea na safari yake." [Musnad Ahmad na al-Hakim. Swaheeh al-Jamee (5545)]

(d) KUKUKUTA KITANDA NA KUEGEMEA UPANDE WA KULIA

Amepokea Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Pindi anapokwenda kulala mmoja wenu na akukute kitanda chake kwa kitambara chake, kwani atakuwa hajui ni kitu gani kilichokuwa juu yake. Kisha na alale kwa upande wake wa kulia..." [Saheeh al-Bukharee na Saheeh Muslim]

(e) KUSOMA ADH-KAAR ZILIZOTAJWA KWENYE SUNNAH KABLA YA KULALA

Kuna idadi ya Adhkaar zilizofundishwa kwenye Sunnah kabla ya kwenda kulala, miongoni mwazo ni kusoma aya za mwisho katika Surat al-Baqarah, kusoma Surat al-Falaq na Surat an-Naas na Surat al-Ikhlaas, kuvuvia kwenye viganja vyako vya mikono kisha kujipangusa kiasi kikubwa uwezacho , kuanzia kwenye kichwa, uso na kisha upande wa mbele wa mwili wako, kwa mara tatu. [Swaheeh al-Bukharee and Swaheeh Muslim]

Amepokea Ali bin Abi Twaalib (رضي الله عنها) yakwamba wakati binti yake Mtume, Faatimah alipomjia Mtume akamtaka amuwekee mtumishi, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia yeye pamoja na Ali: "Kwani nisiwafundishe maneno yatakayokuwa bora kwenu kuliko mtumishi? Munapokwenda kulala, semeni, 'SubhanAllah' mara thalathini na tatu, 'Al-hamdulillah' mara thalathini na tatu, na 'Allahu Akbar' mara thalathini na tatu. Hili ni bora kwenu kuliko mtumishi." [Swaheeh al-Bukharee na Swaheeh Muslim]

5 KUJIEPUSHA NA KULA NA KUNYWA KWA WINGI

Kula na kunywa kupita kiasi ni mojawapo ya vikwazo vyenye kuwafanya watu kuwa ni wavivu na wenye kudharau Qiyaam ul-Layl. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Mtu hajazi chombo chochote kibaya kuliko tumbo lake. Inamtosheleza mwana-adamu kupata tonge zake chache ili ajipatie nguvu anazohitaji. Iwapo anahitaji kujaza tumbo lake, basi na awache kiasi cha thuluthi moja kwa chakula, thuluthi moja kwa kinywaji na thuluthi moja kwa hewa." [Imepokewa na at-Tirmidhee na Ibn Majah. Swaheeh al-Jamee (5674)]

Abu Juhayfah (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia mtu mmoja aliyeteuka mbele yake: "Wacha kuteuka kwako, kwani watu wenye kula sana katika maisha haya ya duniani, ndiwo watakaokuwa na njaa kubwa katika siku ya malipo." [Imepokewa na al-Hakim. Swaheeh al-Jamee (1190)]

6: MTU KUPAMBANA NA NAFSI YAKE

Mtu kupambana na nafsi yake ili aamke na kuswali na kuzikomesha starehe za matamanio ya nafsi yake, ndizo zenye kuleta usaidizi wa Allaah na radhi Zake. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Na ipiganieni Dini ya Allaah kama inavyostahiki (kupiganiwa)..."** [Soorah al-Hajj (22): 78] **"Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini tunawaongoza kwenye njia Zetu. Na bila shaka Allaah Yu pamoja na wafanyao mema."** [al-Ankabut (29): 69]

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mujaahid (mwenye kupigana kwa njia ya Allaah) ni yule mwenye kupambana na nafsi yake kwa ajili ya Allaah." **[**Imepokewa na at-Tirmidhee. Angalia pia as-Swaheehah (549)]

Vilevile amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Anaposimama mtu kutoka katika Ummah wangu kwa ajili ya kuswali swala ya usiku, akajipinda nafsi yake kwa kuamka na kujinadhifisha, huwa kuna mafundo juu yake. Anapo-osha mikono yake pindi aanapotawadha, fundo moja hufunguka. Anapo-osha uso wake, fundo jengine hufunguka. Anapopangusa kichwa chake, fundo jengine hufunguka. Anapo-osha miguu yake, fundo jengine hufunguka. Kisha Allaah atawaambia waliohifadhiwa (kwenye ghaibu): **"Mwangalieni huyu mja wangu, anapambana na nafsi yake na kuniomba Mimi. Chochote aniulizacho mja wangu atakipata."** [Musnad Ahmad. Angalia Swaheeh at-Targheeb (627)]

7: KUJILAUMU NAFSI YAKO KWA KUTOSWALI QIYAAM UL-LAYL

Qiyaam al-Layl ni Baraka kubwa kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى), na akaweka ndani yake faida nyingi za ki-roho na malipo mema kwa waumini. Kwahivyo, mtu inatakiwa ajilaumu mwenyewe iwapo atajikosesha fursa hii kubwa ya kujipatia malipo na radhi za Allaah. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى) katika Qur'an: **"Enyi mlioamini! Mcheni Allaah na kila mtu aangalie, (atazame) anayoyatanguliza kwa ajili ya kesho (Akhera); na mcheni Allaah; hakika Allaah anazo habari za mnayoyatenda (yote)."** [al-Hashr (59): 18]

Amesema Imaam Ibn al-Qayyim (رحمه الله): "Iwapo mja atakuwa ni mwenye kuyabeba majukumu yake na kuwajibika kisawasawa, hata kusikiya kwake, kuona kwake na siri ya moyoni mwake, kama asemavyo Allaah (سبحانه وتعالى): **"… Hakika masikio na macho na moyo; hivyo vyote vitaulizwa."** [Soorah al-Isra (17): 36], kisha na ajitazame yeye mwenyewe kabla hajaletwa kuhukumiwa."

KUNA DARSA ZA WANAWAKE KATIKA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHAAN, MSIKITI WA MAZRUI, KUANZIA SAA NNE ASUBUHI MPAKA ADHUHURI—KILA SIKU ISIPOKUWA SIKU YA IJUMAA.

JAMBO LENYE KUHARIBU SAUMU:

Sindano Zenye Virutubisho

Muradi wa sindano zenye virutubisho ni kule kufikisha vyakula kwa njia za mishipa ili kifike kwenye utumbo, kwa malengo ya kumlisha mgonjwa. Sampuli hii ya sindano huharibu saumu kwani inahusisha kuingiza chakula ndani ya tumbo.

Vilevile, iwapo ile sindano haifiki ndani ya matumbo lakini hufika kwenye damu basi hapo pia huharibu saumu kwa sababu sindano hiyo husimama mahali pa chakula na kinywaji. Wengi katika wagonjwa wenye kuingia kwenye KOMA kwa muda mrefu hupewa chakula kwa kupitia katika sindano yenye glucose na Saline Solution. Mara nyingi hutokea yakwamba wagonjwa walio kwenye koma kwa muda mrefu hulishwa kwa mfano wa matone hayo yenye "glucose" na "saline solution" na vilevile ndivyo itakavyokuwa kwa vivutia-hewa (inhalers) vinavyotumiwa na wenye kuuguwa maradhi ya pumu – hivyo pia huharibu saumu.

(Endelea kutoka Uk. 1)

amesema shughuli za uokoaji zimeripotiwa kuanza tena.

Alisema zilisimamishwa jana usiku kwa sababu ya hali mbaya ya bahari na giza. Mwaka mmoja haujakamilika tangu kutokea ajali nyingine kutoka katika njia hiyohiyo ya meli na kusababisha vifo vya mamia ya watu.